TANGAZO LA SERIKALI NA. 73 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA TAFSIRI YA SHERIA,
(SURA YA 1)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 26(3))*

AMRI YA KUREKEBISHA MAKOSA YA KIUCHAPAJI KATIKA SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI YA MWAKA 2025

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Makosa ya Kiuchapaji Katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2025.

Marekebisho ya makosa ya kiuchapaji Sheria Na. 1 ya mwaka 2024

2. Makosa ya kiuchapaji yaliyomo katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2024 yanarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu cha 65(3) kwa kufuta neno "jimbo" na badala yake kuweka neno "kata"; na

(b) katika kifungu cha 106 kwa kufuta neno "jimbo" lililopo katika maneno yanayofunga kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuweka neno "kata".

Dodoma,
5 Februari, 2025

ONORIUS JOHN NJOLE
*Mwandishi Mkuu wa Sheria*